

HALMASHAURI YA MJI KIBAHA



TANGAZO LA ZABUNI ZABUNI YA UENDELEZAJI WA MUDA ENEO LA WAZI MAILI MOJA(GARDEN) LENYE UKUBWA WA MITA ZA MRABA 2150.

30.05.2022

Halmashauri ya Mji Kibaha inakusudia kutoa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 2150 katika eneo la wazi maili moja kwa ajili ya Ujenzi wa muda(**temporary structure**) kwa vibanda vya kuuza vinywaji, chakula, Nyama choma na Michezo ya watoto.

1. Halmashauri ya Mji Kibaha inapenda kuwaalika watu binafsi, Kampuni, Ushirika, Taasisi au vikundi vilivyosajiliwa kisheria, wenye nia na uwezo wa kuendeleza eneo la wazi kwa ajili ya kuuza vinywaji, chakula, nyama choma na michezo ya watoto na baadae kupangishwa kwa masharti yaliyowekwa na Halmashauri
2. Zabuni zitashughulikiwa kwa utaratibu wa ushindani(**Competitive Bidding**) ulioainishwa kwenye kanuni za manunuzi(**The public procurement-Goods, Works, Non Consultant services and Disposal of Public assets by tender Regulation 2013**) na iko wazi kwa waombaji wanaoishi ndani ya Mji wa Kibaha na mikoa ya jirani
3. Waombaji wote wenye nia na uwezo wanaweza kupata taarifa kamili kupitia Kabrasha za zabuni ambazo zinapatika katika Ofisi ya Katibu wa Bodi ya zabuni Halmashauri ya Mji Kibaha, Kila siku kuanzia saa 2.30 asubuhi hadi saa 9.30 alasiri siku za Jumatatu hadi Ijumaa(kuondoa siku za sikukuu zinazotambulika kitaifa) kuanzia tarehe ya Tangazo hili.

4. Nyaraka ya zabuni inapatikana baada ya kulipia ada ya maombi ya zabuni ya Tsh 30,000 ambayo haitarejeshwa.
5. **Mwombaji awasilishe maombi yatakayoambatana na Mchanganuo wa Gharama za ujenzi wa eneo husika(BoQ),Ramani iliyohakikiwa na Mtaalam,Marejesho ya Fedha kwa Halmashauri kwa mwezi na aeleze atajenga kwa muda gani na baada ya kukamilika atafanya biashara kwa miaka mingapi kabla ya umiliki kurudi Halmashauri**
6. Zabuni zote zifungwe ndani ya bahasha iliyofungwa kwa lakiri(seal) na juu ya bahasha iandikwe maandishi yanayotaja jina la Zabuni "**Zabuni ya Uendelezaji wa muda sehemu ya kuuzia vinywaji,Chakula Nyama choma na Michezo ya Watoto eneo la Wazi Mailimoja(Garden) Kibaha lenye ukubwa wa Mita 2150**" na bahasha hizo zipelekwe Ofisi ya Katibu wa Bodi ya zabuni Halmashauri ya Mji Kibaha.
7. Muda wa mwisho wa kupokea maombi ya zabuni ni tarehe 15.06.2022 siku ya Jumatano saa 4.00 asubuhi.Maombi yote yatafunguliwa muda mfupi baadae na kwamba waombaji wote au wawakilishi wao wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni hizo katika Ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni.
8. Melekezo yote yaliyotolewa katika tangazo hili pamoja na yale yaliyoko katika nyaraka ya zabuni ni sehemu ya masharti kwa mwombaji wa zabuni.
9. Siku ya kutembelea eneo la Mradi(**Site Visit**) ni tarehe **10.06.2022 siku ya Ijumaa saa nne kamili asubuhi**


ENG.MSHAMU A.MUNDE
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI KIBAHA

MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI KIBAHA